

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TUME YA MADINI
MINING COMMISSION



TANGAZO KWA UMMA
PUBLIC NOTICE

Tume ya Madini inapenda kuwatangazia wananchi na wadau wote wa Sekta ya Madini walioko nje na ndani ya Nchi kuwa:

The Mining Commission wishes to announce to the citizens and stakeholders of the mining industry outside and within the country that:

1. Tume ya Madini imeanza zoezi la kuhakiki maombi ya leseni mbalimbali za madini kwa lengo la kutoa leseni hizo kwa maombi ambayo yatakidhi vigezo.

The Mining Commission has begun to review applications of various mining licenses for the purpose of issuing licenses to applications that will meet the criteria.

2. Tume imeanza zoezi hili kwa kupitia na kuhakiki maombi ya leseni yaliyokuwa yamewasilishwa Wizarani kabla ya tarehe 04/07/2017. Hata hivyo Tume inawahakikishia wadau wote kuwa maombi yaliyowasilishwa Wizarani baada ya tarehe hiyo (04/07/2017) nayo yatashughulikiwa ndani ya muda mfupi ujao.

The commission has begun this exercise through reviewing the applications of licenses submitted to the Ministry before 04/07/2017. However, the Commission guarantees all stakeholders that applications which were submitted after (04/07/2017) will be dealt with in the near future.

3. Baada ya kupitia na kuhakiki maombi yaliyowasilishwa kabla ya tarehe 04/07/2017, Tume imeridhia kuwa leseni zifuatazo zitolewe kwa utaratibu ufuatao:

After going through and reviewing applications submitted before 04/07/2017, the Commission has approved the following licenses to be issued in the following order:

3.1 LESENI ZITAKAZOTOLEWA NDANI YA JUMA MOJA KUENZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.

LICENCES TO BE GRANTED WITHIN ONE WEEK FROM DATE OF THIS NOTICE.

- (a) Leseni 1142 za Uchimbaji Mdogo (*Primary Mining Licence - PMLs*) ambazo zimeshalipiwa ada za kuandaa leseni.

1142 Primary Mining Licences whose licence preparation fee has been paid.

- (b) Leseni 399 za wafanyabiashara wa madini za aina ya "*Brokers Licence*" za kipindi kinachoishia Juni 2018.

339 Brokers Licences for Mineral traders for a period ending June 2018.

- (c) Leseni 150 za wafanyabiashara wa madini za aina ya "*Dealers Licence*" za kipindi kinachoishia Juni 2018.

150 Dealers Licences for Mineral traders for a period ending June 2018.

3.2 LESENI ZITAKAZOTOLEWA NDANI YA MWEZI MMOJA BAADA YA TANGAZO HILI.

LICENCES TO BE ISSUED WITHIN ONE MONTH FROM DATE OF THIS NOTICE.

- (a) Leseni 3,252 za Uchimbaji Mdogo (*PMLs*) zitatolewa kwa wahusika baada ya waombaji hao kulipia ada za uandaji wa leseni. Wahusika wanatakiwa kulipa ada hiyo ya uandaji wa leseni ndani ya siku ishirini na nane (28) baada ya tangazo hili. Tume inasisitiza kuwa hizi leseni zitatolewa tu kwa wale waombaji watakaotimiza sharti hilo la malipo ya ada ya uandaji wa leseni.

3,252 Primary Mining Licences (PMLs) will be issued to the relevant applicants after paying for the licence preparation fees. The applicants are required to pay the licence preparation fee within (28) days after date of this announcement. The Commission insists that these licences will only be issued to applicants who will fulfill requirement after paying license registration fee.

- (b) Orodha ya maombi ya leseni yaliyopitishwa katika kifungi (i) na (ii) hapo juu inapatikana katika Ofisi za Madini za Kanda husika hivyo waombaji wa leseni hizo wanatakiwa kwenda kwenye ofisi za Kanda kwa maelekezo zaidi.

A list of approved licence applications as provided under items (i) and (ii) above is available in the relevant Regional Offices Office, therefore applicants of the said licences are required to go to Regional Offices for further instructions.

3.3 UTOAJI WA LESENI ZA KATI ZA UCHIMBAJI MADINI (MINING LICENCES – MLs) NA LESENI ZA UTAFUTAJI MADINI (PROSPECTING LICENCES – PLs)

GRANT OF MINING LICENCES (MLs) AND PROSPECTING LICENCES (PLs)

- (a) Tume imepitia pia maombi ya leseni za Uchimbaji wa Kati (*Mining Licences – MLs*) na Utafutaji wa Madini (*Prospecting Licences – PLs*) na kufikia uamuzi ufuatao:

The Commission has also reviewed Mining Licenses - MLs and Prospecting Licenses - PLs and reached the following decision:

(b) Leseni za Uchimbaji wa Kati (MLs)

Mining Licences (MLs)

(i) Leseni 8 za Uchimbaji wa Kati zilizokidhi vigezo zitolewe.

8 Mining Licences which have met all the requirements to be granted.

(ii) Leseni 7 za Uchimbaji wa Kati zitolewe baada ya waombaji husika kukamilisha michakato ya kisheria kuhusiana na leseni zao (*amalgamation of PMLs and conversion to MLs as well as Resolutions of Pending Disputes*).

7 Mining Licenses shall be issued after applicants have completed legal requirements regarding their licenses.

(c) Leseni za Utafutaji Madini (PLs)

Prospecting Licences (PLS)

(i) Leseni 88 za Utafutaji Madini (*PLs*) ambazo zimeshalipiwa ada za utayarishaji wa leseni zitolewe kwa waombaji.

88 Prospecting Licences (*PLs*) whose licence preparation fees has been paid for to be granted to applicants.

(ii) Leseni 62 za Utafutaji Madini (*PLs*) zitolewe baada ya waombaji kukamilisha malipo ya ada ya utayarishaji wa leseni husika.

62 Prospecting Licences (*PLs*) should be issued after applicants have completed payment of licence preparation fee for the respective licences.

4. Pamoja na kuridhia utoaji wa leseni za Uchimbaji wa Kati (15) na za Utafutaji Madini (150) zilizoainishwa kwenye kifungu (iii) cha tangazo hili, Tume inawakumbusha waombaji wa leseni hizo kuwa wanatakiwa kuwasilisha kwa mujibu wa sheria maandiko maalumu yanayoainisha mipango yao ya Ushiriki wa Wazawa na utoaji huduma kwa Jamii (*Local Content*) ikijumuisha mipango ya wajibu wa Kampuni kwa Jamii (*Corporate and Social Responsibilities*) pamoja na Tamko la Kiapo cha Uadilifu (*Integrity Pledge*). Tume inasisitiza kuwa hakuna leseni hizi kubwa itakayotolewa bila muombaji kutekeleza na kukamilisha matakwa hayo ya kisheria.

In addition to authorising the grant of 15 Mining Licences and 150 Prospecting Licences as provided under item (iii) of this notice, the Commission reminds license applicants, that they are required to submit in accordance with the law, special policy that outlines local content involvement and community services, including Corporate and Social Responsibilities plans as well as the Integrity Pledge. The Commission emphasizes that no major licenses will be provided without the applicant fulfilling these legal requirements.

5. Orodha ya maombi ya leseni hizi Kubwa na za Kati yaliyopitishwa inapatikana katika Ofisi za Wizara ya Madini, Dodoma hivyo waombaji wa leseni hizo wanatakiwa kwenda kwenye ofisi Wizara kwa maelekezo zaidi.

The list of approved applications for Prospecting Licences (PLs) and Mining Licences (MLs) is available at the Ministry of Minerals, Dodoma, so that applicants should go to the Ministry for more instructions.

Prof. Idris Suleiman Kikula

MWENYEKITI WA TUME YA MADINI

18 Mei, 2018